

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

Simu Na: +255 (026) 2740016

Nukushi: +255 026 2740103

Barua Pepe: ded@maketedc.go.tz

Tovuti: <http://www.maketedc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Makete,
S. L. P 6,
MAKETE.

Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na. EA.172/302/01/161

26 Mei, 2022

TANGAZO LA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mpya chenye Kumba NaFA.97/228/01/9 cha tarehe 13/Mei/2022 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia Watanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi ya kazi kama ifutavyo:-

1. KATIBU MAHSUSI Daraja III-NAFASI 3

1.1 Sifa za Mwombaji

- Awe mwenye elimu ya kidato cha nne au sita
- Awe na Astashahada (NTA Level 5) ya Mafunzo ya uhazili na kufaulu Mtihani wa hatua ya tatu
- Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kingereza Maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) au Chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

1.2 MAJUKUMU

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka mbalimbali.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.

- c. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- d. Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- e. Kusaidia kufikisha maelekezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- f. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- g. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Muundo na Ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani **TGS B1 kwa mwezi**.


1.4 MASHARTI YA WAOMBAJI WOTE

- I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- II. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- III. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referecs) watatu wa kuaminika.
- IV. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - a. Cheti cha Taaluma
 - b. Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita
 - c. Cheti cha kuzaliwa
 - d. Nakala ya kitambulisho cha NIDA
 - e. Picha mbili za Passport size za hivi karibuni.

- V. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo ya kidato cha nne au sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
- VI. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza
- VII. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimchakikiwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- VIII. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 08, Juni, 2022 saa 9:30 Alasiri. Baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa, na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.maketecd.go.tz na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.
- IX. Muhimu, kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zile zinazihitajika. Barua ya maombi itumwe kwa;

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Makete,
S.L.P. 6,
MAKETE.**

Tangazo limetolewa na:



William M. Makufwe
Mkurugenzi Mtendaji (W)
MAKETE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MAKETE

Nakala: Mbao za Matangazo
Halmashauri ya Wilaya,
MAKETE.